# MAPITIO YA MWENENDO WA SOKO KWA WIKI
# 22 NOVEMBA 2024

**KARIBUNI TENA KATIKA KIPINDI CHETU CHA KILA WIKI KINACHOKUHABARISHA KUHUSU MWENENDO WA SOKO LA HISA LA DAR-ES-SALAAM, NA KULETWA KWENU NA VERTEX INTERNATIONAL SECURITIES, PAMOJA NANYI LEO NI MIMI, FRANCO ATILYO**

Kwa wiki inayoishia tarehe 22 Novemba 2024, mauzo katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) yaliongezeka kwa kiasi cha asilimia 56.08, kutoka TZS 1.41 bilioni hadi TZS 2.2 bilioni. kiasi cha hisa zilizouzwa pia kilipanda kwa asilimia 68.76 kutoka hisa milioni 1.17 hadi hisa milioni 1.98.

Jumla ya Mtaji wa Soko ulipungua kwa asilimia 0.65, kutoka TZS 18.38 trilioni hadi trilioni 18.26. Mtaji wa Soko la Ndani pia ulipungua kwa asilimia 0.64, hadi TZS 12.21 trilioni kutoka TZS 12. 29 trilioni kutokana na kupungua kwa bei ya TPCC, NICO, na DSE.

CRDB imeongoza kwa mauzo ya hisa wiki hii ikirekodi TZS 1.11 bilioni, ambayo ni 50.37% ya mauzo yote ikifuatiwa na NMB iliyorekodi TZS 1.02 bilioni, sawa na asilimia 46.57 ya mauzo yote.

Kwa upande wa bei, AFRIPRISE ilipanda kwa TZS 5 na CRDB ziliongezeka kwa TZS 30. Hisa za NMB nazo ziliongezeka bei kwa TZS 100 huku hisa za SWISS zikiongezeka pia kwa TZS 120. Hisa TCCL ziliongezeka kwa TZS 60 na zile zqa TOL nazo pia ziliongezekakwa TZS 20. Hisa za DSE na NICO zilishuka bei kwa TZS 60 kila moja, za TPCC zilishuka kwa TZS 220.

Jumla ya hisa laki sita za NMB na hisa laki tano za CRDB ziliuzwa kupitia kaunta ya makubaliano ya kabla huku wawekezaji wa ndani wakiendelea kutawala mauzo ya soko wakirekodi jumla ya TZS 2.18 bilioni. Tunatarajia kuongezeka kwa mwitikio utakaoakisi kwenye mauzo ya hisa na bei kwa wiki ijayo.

Katika wiki kulikuwa na miamala 118 kwenye soko la hatifungani, ambapo soko lilisajili takribani TZS 16.2 bilioni.

Mnada wa Hatifungani za muda mfupi uliofanywa tarehe 20 Novemba 2024, ulivutia zabuni 76 ambapo zabuni 34 zilifaulu. Jumla ya fedha zilizopatikana ni TZS 4.9 bilioni.

# MAPITIO YA MWENENDO WA SOKO KWA WIKI
# 22 NOVEMBA 2024

**MPAKA HAPO TUMEFIKIA MWISHO WA MAPITIO YA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM KWA WIKI ILIYOISHIA IJUMAA YA NOVEMBA 22, 2024. MPAKA WAKATI MWINGINE MIMI NI FRANCO ATILYO**